

Nini cha Kuleta Hospitali Wakati wa Kuzaa Mtoto



What to Bring to Hospital when Having a Baby

Swahili

July 2022

Hii ni orodha ya mapendekezo ya vitu vya kuletea hospitali kwa kuzaliwa kwa mtoto wako.

Kwa gari

- Taulo 2 safi za zamani
- Chombo cha plastiki katika kesi ya kutapika

Tafadhali hakikisha kuwa una kizuizi cha gari kilichoidhinishwa kilichowekwa, kwa ajili ya mtoto wako kwenye gari lako kabla ya uchungu wa uzazi (leba).

Utahitaji

- Kadi yako ya mjamzito
- Kadi ya Medicare
- Maelezo ya bima (ikiwa unayo)
- Nguo ya kuvaa wakati unapokuwa na uchungu wa uzazi – t-shati kubwa au vazi kuu la kulalia
- Mavazi ya usiku na kanzu ya kulala
- Nguo za mchana zilizolegea na zinazostarehesha
- Viatu vya kustarehesha
- Nguo za ndani ikiwa ni pamoja na sidiria 2 za kunyonyesha. Wanawake wengine hutumia chupi cha kutupwa
- Pedi za usafi za ukubwa wa uzazi
- Pedi za matiti au kunyonyesha
- Vifaa vya usafi - sabuni, mswaki, dawa ya meno, kiondoa harufu, shampuu, brashi, kitana na kitambaa cha uso.
- Mafuta ya mdomo
- Kikaushia nywele
- Mapipi ya kunyonya
- Chaja ya simu

Kwa wenzi na watu wasaidizi

- Chakula, vitafunio na vinwaji
- Nguo za kustarehesha na sweta kwani hospitali ina kiyoyozi
- Kalamu na karatasi inaweza kufaa
- Mavazi ya kuogelea
- Simu iliyo na kamera/vidio, kamera au rekoda ya vidio na chaja

Kwa mtoto mchanga

- Nepi (8-10 kwa siku)
- Kifuta cha mtoto mchanga
- Ikiwa unapanga kulisha mtoto wako maziwa ya unga, utahitaji kuleta unga wa maziwa wako na chupa
- Nguo za mtoto za kuvaa anapoenda nyumbani

Je, vipi nikihitaji usaidizi wa kuzungumza Kiingereza?

Wakalimani wa kitaalamu wanapatikana ikiwa unahitaji usaidizi wa kuelewa au kuzungumza kwa Kiingereza. Huduma za mkalimani ni za bure na za siri. Ikiwa ungependa mkalimani tafadhali waulize wafanyakazi au piga simu kwa Huduma ya Utafsiri na Ukalimani (TIS) kwa 131 450.

Local Contact (Mawasiliano wa karibu)

Person's name (Jina): _____

Contact number (Simu): _____